WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA TANZANIA

## KIPINDI CHA OKTOBA - DESEMBA 2016

**Dondoo muhimu za msimu wa mvua kipindi cha Oktoba-Disemba 2016**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua katika kipindi cha Oktoba - Disemba 2016 na athari zake kwa sekta mbali mbali zinazohitaji zaidi taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yake kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na wanyamapori, maliasili na utalii, nishati na maji, mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:-

**a) Mwelekeo wa msimu wa mvua kipindi cha Oktoba - Disemba 2016:**

- Kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2016 mvua chache zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi, wakati maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Viktoria pamoja na yale ya kusini mwa nchi mvua zinatarajiwa kuwa za kuridhisha.
- Katika maeneo mengi nchini mvua zinatarajiwa kuchelewa kuanza. Aidha, mvua hizi zinatarajiwa kuanza katika ukanda wa Ziwa Viktoria na pia katika maeneo machache ya pwani ya Kaskazini katika mwezi Oktoba, 2016.

**b) Athari na Ushauri**

- Vipindi virefu vikavu ndani ya msimu wa mvua vinatarajiwa kusababisha unyevunyevu mdogo katika udongo na hivyo kupelekea kuathiri ustawi wa mazao ya kilimo katika maeneo mengi ya nchi.
- Kutokana na mtiririko mdogo wa maji vina vya mito na mabwawa vinatatarajiwa kupungua kutoka katika hali yake iliyopo katika kipindi cha msimu wa Vuli, 2016 kutokana na mvua chache zinazotarajiwa katika maeneo mengi.
- Uwezekano wa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanatarajiwa kupelekea mafuriko katika maeneo machache na hususani katika maeneo yasiyo na uoto mwingi.
- Milipuko ya magonjwa inaweza kujitokeza kutokana na uhaba wa maji salama na matumizi mabaya ya mifumo ya maji taka katika miji.
- Uhaba wa malisho kwa mifugo na wanyama unatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi kutokana kupungua kwa maji katika mabwawa na visima.



## (I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA - DISEMBA 2016

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa iliyopo na inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele II cha taarifa hii), kuna uwezekano mkubwa wa uhaba wa mvua na mtawanyiko hafifu katika kipindi cha msimu wa mvua wa Oktoba hadi Disemba 2016. Maeneo ya pwani ya Kaskazini pamoja na yale ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki yanatarajiwa kuwa na vipindi virefu vikavu. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa msimu wa mvua ni kama ifuatavyo:

### 1 *Mvua za Vuli 2016 (kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua)*

Msimu wa mvua za Vuli 2016 ni mahususi katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki, pwani ya Kaskazini na visiwa vya Unguja na Pemba, ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua za kipindi cha Oktoba - Disemba 2016 zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani kwa maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Viktoria. Maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Viktoria, pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki yanatarajiwa kuwa na mvua za chini ya wastani hadi wastani.

Kuanza kwa mvua za Vuli 2016 kunatarajiwa kuchelewa katika maeneo mengi na vipindi vikavu vinatarajiwa katika maeneo mengi hususani katika miezi ya Oktoba na Novemba, 2016.

***1.1 Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):***

Mvua zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya mkoa wa Kagera mnamo wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba, 2016 na kusambaa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Simiyu na Shinyanga kufikia wiki ya tatu ya mwezi Oktoba, 2016. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani isipokuwa katika maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Viktoria hususan mikoa ya Kagera, Mwanza na Geita ambapo mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa.

***1.2 Ukanda wa Pwani ya Kaskazini:*** (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):

Maeneo ya mkoa wa Tanga mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Oktoba, 2016 na kusambaa katika maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam, visiwa Unguja na Pemba na kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2016. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi hususani katika miezi ya Oktoba na Novemba, 2016.



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706

***1.3 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki:*** (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2016 na zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi.

## 2 Mvua za Msimu (Novemba – Aprili) kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua.

Msimu wa mvua za Novemba hadi Aprili ni mahususi kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Magharibi mwa nchi, kanda ya kati, Nyanda za Juu Kusini-magharibi, kusini mwa nchi na pwani ya Kusini). Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuchelewa kuanza katika maeneo mengi. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi isipokuwa maeneo ya pwani ya Kusini, hususani katika maeneo ya mkoa wa Mtwara na kusini mwa mkoa wa Lindi na kusini-mashariki mwa mkoa wa Ruvuma, ambapo mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa.

### 2.1 Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa):

Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2016 katika mkoa wa Kigoma na kusambaa katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Tabora katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2016 na kwa ujumla mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani.

### 2.2 Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya Mwezi Disemba, 2016 na zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi.

### 2.3 Nyanda za juu Kusini Magharibi: (Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na kusini mwa Morogoro):

Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Disemba, 2016 na zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi.

### 2.4 Maeneo ya kusini na pwani ya kusini (Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara)

Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Disemba, 2016 na zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi isipokuwa katika maeneo ya mkoa wa Mtwara na kusini mwa mkoa wa Lindi na kusini-mashariki mwa mkoa wa Ruvuma, ambapo mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa.

| MWELEKEO WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA-DISEMBA 2016 | WASTANI WA MVUA WA MUDA MREFU (mm) OKTOBA – DISEMBA 2016 |
|---|---|
|   |   |

*Picha 1 – Ramani ya wastani wa mvua – kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba; Kushoto: Mwelekeo wa mvua katika msimu huu wa Oktoba hadi Disemba 2016.*

***Angalizo:***

*Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani na chini ya wastani.*

## (II) MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya Joto la chini ya wastani iliyopo katikati mwa eneo la Kiikweta la Bahari ya Pasifiki na Magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) inatarajiwa kuendelea kuwepo katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2016 ambapo katika eneo la Mashariki mwa Bahari ya Hindi (Indonesia) hali ya joto la juu ya wastani iliyopo inatarajiwa kuendelea katika kipindi cha msimu wa vuli.

Hali hii ya mfumo wa joto inaashiria kuwepo kwa upepo wenye unyevunyevu hafifu kutoka Mashariki kuelekea pwani ya Afrika Mashariki. Hali ya joto la chini ya wastani katika Bahari ya Pasiki imepewa jina la La Niña. Aidha, hali ya mfumo huu wa upepo unatarajiwa kusababisha upungufu wa mvua katika maeneo ya Kaskazini na yale ya Kaskazini-mashariki mwa nchi. Hata hivyo, katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi joto la wastani linatarajiwa kuwepo

kuelekea mwezi Disemba, 2016 na hivyo kupelekea kuchelewa kuanza kwa mvua katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua.

Kuongezeka kwa joto katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola, hususani katika miezi ya Oktoba na Disemba, 2016 kunatarajiwa kusababisha kuwepo na upepo wenye unyevunyevu hafifu kutoka katika misitu ya Kongo kuelekea katika maeneo ya Magharibi, Kusini-magharibi na katikati mwa nchi na hivyo kusabisha upungufu wa mvua katika maeneo hayo. Hali ya joto la wastani katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi katika miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2016 inatarajiwa kupunguza matukio ya vimbunga na hivyo kusababisha mvua chache katika msimu wa Vuli.

## (III) ATHARI NA USHAURI

### Kilimo na Usalama wa Chakula

Katika maeneo mengi ya nchi msimu wa mvua kipindi cha Oktoba-Disemba 2016 mvua zinatarajiwa kuchelewa kuanza na zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuwa si ya kuridhisha kwa ustawishaji wa mazao ya kilimo na malisho ya mifugo. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba na pembejeo mapema pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani wa kilimo kwa matumizi sahihi ya ardhi na mbegu. Aidha, wakulima wanashauriwa kutumia kwa uangalifu na kuhifadhi akiba ya chakula waliyonavyo.

### Malisho, Maji kwa ajili ya mifugo na Wanyama pori

Upungufu wa malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na wanyama pori unatarajiwa katika maeneo mengi ambayo mvua za chini ya wastani zinatarajiwa. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kuhifadhi chakula kwa ajili ya malisho ya mifugo. Aidha, wafugaji wanashauriwa kuvuna mifungo ikiwa katika hali nzuri kiafya. Maeneo ambayo mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa wakulima wanashauriwa kuzalisha na kuhifadhi malisho ya kutosha ili yatumike katika kipindi cha upungufu wa mvua. Milipuko ya magonjwa inatajariwa katika kipindi cha msimu hivyo inashauriwa mifugo na wanyama kufanyiwa chanjo za mara kwa mara.

Matukio ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo, wanyamapori na shughuli nyingine za kiuchumi yanatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo ambayo mvua za chini ya wastani zinatarajiwa kwa wanyama pori

kuingia katika mashamba ili kujitafutia malisho. Hivyo, Mamlaka za wanyama pori pamoja na jamii iishio katika maeneo hayo wanashauriwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya migogoro ambayo inaweza kujitokeza. Katika maeneo mengi ya nchi ambapo mvua za chini ya wastani zinatajariwa, kutakuwa na upungufu wa malisho kwa ajili ya wanyamapori hivyo hatua mbadala zichukuliwe kupunguza athari.

## Maliasili na Utalii

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, Mamlaka za usimamizi wa shughuli za utalii na hifadhi za wanyamapori zinashauriwa kuchukua hatua stahiki. Hatua hizo ni pamoja na kuzuia uharibifu wa miundombinu kama vile barabara na madaraja ndani ya hifadhi dhidi ya athari za vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyoweza kujitokeza katika kipindi cha msimu wa vuli 2016.

### Maji na Nishati

Kwa vile mabwawa mengi yako katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani, upungufu wa maji kwenye mabwawa unatarajiwa kutokea, hivyo inashauriwa maji yaliyopo yatumike kwa uangalifu. Upungufu wa nishati ya umeme wa maji unaweza kujitokeza hivyo njia mbadala za uzalishaji wa nishati ya umeme zinashauriwa zitumike. Wananchi wanashauriwa kuzingatia taratibu za uvunaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali maji.

### Mamlaka za Miji

Mamlaka za miji pamoja na wananchi wanashauriwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanyakazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kupelekea mafuriko na uharibifu wa miundombinu. Aidha, hatua hizo zichukuliwe hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani kwa sababu vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza.


Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706

**Sekta ya Afya**

Kutokana na uhaba wa maji salama unaotarajiwa kwa shughuli za binadamu ikiwemo usafi wananchi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia milipuko ya magonjwa. Aidha Sekta ya Afya inashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

**Menejimenti ya Maafa**

Mamlaka za maafa na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utunzaji wa mazingira, upatikanaji wa maji safi na salama, na usambazaji wa madawa, maji na chakula ikiwa ni hatua za kujiandaa na kukabiliana na majanga yanayoweza kutokea kutokana na vipindi vya mvua za chini ya wastani zinazotarajiwa.

**Vyombo vya habari**

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii. Aidha, jamii nayo inashauriwa kufuatilia na kuzingatia taarifa sahihi za hali ya hewa na mirejeo yake kupitia vyombo vya habari.

Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

*Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

***Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania Itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.***

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi
**Mkurugenzi Mkuu**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706